



P. O. BOX 349, SHINYANGA, TEL/FAX 255 28 2762525
Email:info@shireculimited.co.tz Website:www.shireculimited.co.tz

KUMB. NA.SRCU/TB/39/VOL.II/26

TAREHE: 30/01/2025

A. TANGAZO LA ZABUNI

- Chama kikuu cha Ushirika Mkoa wa Shinyanga ni Chama kilichosajiliwa kwa **Na.AFF-SHY-SHY-MC-2022-9** na hufanya kazi chini ya sheria ya Vyama vya Ushirika Namba **6** ya mwaka **2013** pamoja na kanuni zake za mwaka **2015**. Maeneo ya shughuli za Chama hiki ni Mkoa wa Shinyanga katika Wilaya ya Shinyanga Mjini, Shinyanga Vijijini na Kishapu.
- Kwa idhini ya Bodi ya chama Kikuu, Mwenyekiti wa bodi anatangaza zabuni shindanishi ya Kitaifa (National Competitive Tendering) kwa zabuni ya uendeshaji wa Maghala.

B. MAHITAJI YA ZABUNI

ZABUNI NA.	MAELEZO YA ZABUNI
SRCU/2024-2025/ZBN/UGL/01	Zabuni ya ukodishaji wa Maghala kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025
SRCU/2024-2025/ZBN/UGL/02	Zabuni ya Usafirishaji

Chama kinatangaza **ZABUNI YA MWENDESHA GHALA NA ZABUNI YA USAFIRISHAJI** kwa mazao ya jamii ya mikunde yaani Choroko, Dengu, Alizeti na Mpunga kutoka kwenye vituo vya Vyama vya Msingi **[AMCOS]** vilivypo katika Halmashauri za Kishapu, Shinyanga **DC** na Manispaa hadi kwenye Maghala Makuu ya Minada yaliyopo Mhunze Jineri Wilaya ya Kishapu na Uzogore Jineri Wilaya ya Shinyanga Mjini.

- Mzabuni mmoja anaruhusiwa kuomba ghala zaidi ya moja endapo atakuwa amethibitisha kuwa na uwezo.
- Mchakato wa zabuni hii utafanyika kwa njia shindanishi ya kitaifa (National Competative Tendering) kwa mujibu wa Mwongozo wa Ununuzi na Ugavi wa vyama vya Ushirika Tanzania Bara na Sheria na Kanuni za ununuzi wa umma na nizabuni ya wazi kwa wazabuni wote wenye sifa zinazohitajika.
- Kitabu cha zabuni kinapatikana baada ya kulpia ada ya Zabuni kwa gharama ya Fedha ya Kitanzania Shilingi Laki moja tu (100,000) ambazo hazitarudishwa. Fedha zote zilipwe kwenye AKAUNTI NAMBA **01J1058431301** jina la Akaunti **SHIRECU (1984) LTD Benki ya CRDB**. Ukishalipa njoo na bank slip (uthibitisho wa malipo)
- Waombaji wawasilishe zabuni zao (Nakala mbili) nakala halisi moja na kopi moja zikiwa zimefungwa kwenye bahasha kwa umakini na kutiwa lakiri.

- 7. Muda wa kutuma maombi ya Zabuni ni siku sita 6 baada ya Tangazo kutolewa kuanzia tarehe 30 January, 2025 hadi tarehe 7 february, 2025 saa Nne kamili asubuhi na SIKU HIYO NDIO SIKU YA UFUNGIZI.
- 8. Zabuni zitakazochelewa hazitapokelewa wala hazitafanyiwa kazi wakati wa tathimini ya Zabuni bila kujali sababu zozote za kuchelewa kwao.

C. SIFA ZA JUMLA ZA MWOMBAJI

- i. Awe Mmiliki wa Kampuni iliyosajiliwa na **BRELA** na yenyenamba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi [**TIN**]
- ii. Kampuni iwe na uwezo na uzoefu wa kuendesha shughuli za Maghala.
- iii. Kampuni iwe na watumishi wenye uwezo na sifa kutoka **BODI** ya Maghala.
- iv. Kampuni iwe na vitendea kazi kama vipima unyevu [**Moisture meter**], Chekecheo la maabara na Pallets za kutosha.
- v. Kampuni iwe na Leseni hai ya kuendesha Shughuli za Maghala.
- vi. Kampuni iwe haijawahi kusababisha hasara katika kazi zake.
- vii. Kampuni iwe tayari kusajili Ghala Mhunze Jineri-Kishapu na Uzogore Jineri-Shinyanga Mjini.
- viii. Kampuni iwe na cheti cha usafirishaji.
- ix. Waombaji wawe na kitambulisho cha NIDA.

MAOMBI YOTE YAANDIKWE KWA KUZINGATIA YAFUATAYO:

Tarehe ya mwisho kuwasilisha maombi ni siku ya **Ijumaa, Februari 7, 2025** saa **4:00 asubuhi (Saa nne kamili asubuhi)** na **SIKU IYO ITAKUWA NI SIKU YA UFUNGIZI (saa Nne Asubuhi Kamili)** itakuwa siku ya ufunguzi utakaofanyika Makao makuu ya Ofisi ya Chama kikuu cha Ushirika [**SHIRECU (1984) LTD**], Waombaji wote mnashauriwa kuhudhuria wenyewe bila kutuma wawakilishi.

Maombi ya Zabuni yatakayowasilishwa Ofisi ya Chama kikuu [**SHIRECU (1984) LTD**] yafungwe ndani ya bahasha kwa **LAKIRI** au kutumwa kwa barua pepe info@shireculimited.co.tz yakiwa katika faili moja aina ya PDF.

Barua iandikwe kwa;

**KAIMU MENEJA MKUU,
SHIRECU (1984) LTD,
S. L. P. 349,
SHINYANGA.**

Asnath Changamike
**SHIRECU <1984> LTD
P. O. Box 349
SHINYANGA
TANZANIA**

**KAIMU MENEJA MKUU
[SHIRECU (1984) LTD]**